

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA KUMI NA TISA**

**29 APRILI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 29 APRILI, 2021**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**158. MHESHIMIWA SIMON SONGE  
LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Kata ya Imalamate Wilayani Busega wamejenga Zahanati na kumaliza maboma manne kwa maana ya Zahanati moja kila Kijiji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wananchi hao kuezeka maboma hayo ili waweze kupata huduma za Afya kwenye Zahanati hizo.

#### OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

**159. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS  
(KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mto Msimbazi ambao umeainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **160. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Jimbo la Namtumbo lina tatizo la maji karibu maeneo yote ya Vijijini pamoja na Makao Makuu ya Wilaya:-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili katika Bajeti ya Mwaka 2020/2021.



## **WIZARA YA KILIMO:**

### **161. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mabwawa makubwa na Skimu za Umwagiliaji za Choma Chankola, Ziba na Simbo ambazo zimefanywa upembuzi yakinifu kwa zaidi ya miaka sita sasa.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **162. MHESHIMIWA MWANTUMU MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-  
Usambazaji wa umeme Vijijini unapaswa  
kukamilika ifikapo Mwaka 2021/2022:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha  
kuwa usambazaji wa umeme Vijijini  
unakamilika kama ilivyopangwa.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya  
Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA  
29 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**